



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO  
YA UFUNDI STADI



MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe \_\_\_\_\_ mwezi \_\_\_\_\_ 2022

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha MARA - VIC, S.L.P. 188,

MUSOMA ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802 DODOMA (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

SAMWEL MAIGA MIANI S.L.P. 13, BUTIAMA

(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundu") kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya BUTIAMA;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya BUTIAMA;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundu kwa ajili ya kazi ya SKIMMING & PAINTING - BWEMI LA WASICHANA

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundu nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinayoonesha namna kazi itakavyofanyika;

**HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

**1. GHARAMA YA UFUNDI**

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 1,800,000.00, Fundi atafanya kazi ya SKIMMING & PAINTING kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

**2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)**

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapo kuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

**3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO**

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

(a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi

(b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundi;

(c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundi;

(d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80: 30% ya Gharama ya Ufundi;

(e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundi; na

(f) Baada ya kukamilika kwa "Muda wa matazamio": 5% ya Gharama ya Ufundi.

**4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI**

(a) Fundi atakabidhiwa eneo la tarehe 20 mwezi 02 2022

au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.

(b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 30 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.

(c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

**5. WAJIBU WA FUNDI**

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kujenga SKIMMING & PAINTING na kukamilisha ujenzi kama inavyoonekana katika Michoro pamoja na Mchanganuo wa Vifaavya Ujenzi (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA  
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA YETA-  
MARA.

Jina: DAVID L. BENEDICT Saini: \_\_\_\_\_

Wadhifa: MSIMAMAZI WA MRADI  
BUTAMA DVTC Tarehe: \_\_\_\_\_

Mbele ya (Shahidi)

Jina: ALFRED G. KIDIFU Saini: \_\_\_\_\_

Wadhifa: AFISA MANUNUZI Tarehe: \_\_\_\_\_

IMESAINIWA NA FUNDI

Jina: SAMUEL MAIGA NTAN Saini: \_\_\_\_\_

Wadhifa: FUNDI MKUU Tarehe: \_\_\_\_\_

Mbele ya (Shahidi)

Jina: AMONI CHUMA Saini: \_\_\_\_\_

Wadhifa: FUNDI MSAIBIZI Tarehe: \_\_\_\_\_

*[Signature]*  
VTC MANAGER  
MARA VTC  
P.O. BOX 188  
MUSOMA

*[Signature]*  
14/02/2022  
DEPARTMENT OF LOGISTICS OFFICER  
MARA VTC  
P.O. BOX 188  
MUSOMA - MARA

*[Signature]*

24:02:2022

*[Signature]*

14:02:2022